

**MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI (CMT)  
KILICHOFANYIKA TAREHE 10/05/2022 KATIKA UKUMBI WA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA KWA AJILI YA KUPITIA  
TAARIFA MAPATO NA MATUMIZI**

"KIZIDUO"

**MAHUDHURIO:**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

1.	Ndg. Julius Mulongo	Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)	Mwenyekiti
2.	Ndg. Rebecca Samwel	Kaimu Afisa Raslimali watu (W)	Katibu
3.	Ndg. Ogedjo Aila	Mkaguzi wa Ndani (W)	Mjumbe
4.	Ndg. Mudricat H. Rukazibwa	Afisa Ardhi na Maliasili (W)	Mjumbe
5.	Ndg. Aliko A. Ndile	Kaimu Afisa Nyuki (W)	Mjumbe
6.	Ndg. Nestory Mjojo	Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)	Mjumbe
7.	Ndg. Paul Misana	Afisa Uchaguzi (W)	Mjumbe
8.	Shija Lyela	Afisa Mifugo na Uvuvi (W)	Mjumbe
9.	Ndg. Magreth P. Stephano	Kaimu Mwanasheria (W)	Mjumbe
10.	Ndg. Kinyemi Sepeku	Afisa Elimu Msingi (W)	Mjumbe
11.	Ndg. Yohana Nyiganda	Kaimu Afisa Usafishaji na Mazingira (W)	Mjumbe
12.	Ndg. Rehema Katany	Kaimu Mganga Mkuu (W)	Mjumbe
13.	Ndg. Nasibu Lucas	Kaimu Afisa Ugavi (W)	Mjumbe
14.	Ndg. Mohamed Mavura	Kaimu Afisa TEHAMA (W)	Mjumbe
15.	Ndg. Charles Matiku	Mweka Hazina (W)	Mjumbe
16.	Ndg. Rajabu H. Mfinanga	Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)	Mjumbe

17. Ndg. Elizabeth Shirima

Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)

Mjumbe

**SEKRETARIATI:**

1. Ndg. Christa D. Manyalla

Sekretarieti

2. Ndg. Happy D. Kalingo

Sekretarieti

**MUHTASARI NA 68/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu wa kikao alimkaribisha mwenyekiti ili aweze kufungua kikao baada ya kujiridhisha na akidi ya wajumbe kwenye kitabu cha mahudhurio.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao cha kawaida kwa ajili ya kupitia taarifa ya mapato na matumizi kuishia tarehe 31/04/2022. Alifungua kikao mnamo saa 2:08 asubuhi.

**MUHTASARI NA 69/2021/2022: KURIDHIA AGENDA**

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia agenda zilizoandaliwa kwa ajili ya kikao kama ifuatavyo;

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia Agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichofanyika tarehe 8/02/2022
4. Yatokanayo na kikao kilichofanyika tarehe 8/02/2022
5. Taarifa ya mapato na matumizi kuishia tarehe 31/04/2022
6. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya UVIKO-19 ujenzi wa Nyumba ya Watumishi (3 In 1) katika Kituo cha Afya Maisome na Jengo la dharura (EMD) katika Hospitali ya Isaka
7. Kugunga Kikao

**MUHT. NA. 86/2021/2022: 6. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UVIKO-19 UJENZI WA NYUMBA YA WATUMISHI (3 IN 1) KATIKA KITUO CHA AFYA MAISOME NA JENGO LA DHARURA (EMD) KATIKA HOSPITALI YA ISAKA**

DMO aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya UVIKO-19 ya Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya UVIKO-19 ujenzi wa Nyumba ya Watumishi (3 In 1) katika Kituo cha Afya Maisome lenye thamani ya Tsh. 90,000,000.00 na JenGO la dharura (EMD) katika Hospitali ya Isaka yenye thamani ya Tshs 300,000,000.00 Wajumbe walipokea na kupongeza kwa utekelezaji mzuri wa ujenzi wa majengo hayo yanayogarimu kiasi cha Tsh. 390,000,000.00

*(Taarifa imeambatanishwa)*

Wajumbe walipokea na kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha hizo ambazo zimepunguza uhaba wa majengo ya kutolea huduma za Afya.


**MUHT. NA. 87/2021/2022: KUFUNGA KIKAO**

Katibu wa kikao alimkaribisha mwenyekiti ili afunge kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote kwa mawazo na kusisitiza yote yaliyojadiliwa yafanyiwe kazi. Alifunga kikao muda wa saa 5:34 asubuhi

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

  
.....  
KATIBU

  
.....  
MWENYEKITI

TAREHE.....17/05/2022.....

